# Wafugaji washauriwa kupeleka watoto shule

Na Doreen Aloyce, Dodoma

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka amewataka wafugaji kuwapeleka watoto wao shule na kuacha utaratibu wa kuwafanya kuwa ndiyo wachungaji wa mifugo.

Pia alisema mfugaji kuwa na mifugo mingi ni utajiri, hivyo wanatakiwa kufuga kwa tija ili iweze kuwanufaisha ikiwa ni pamoja na kuwapeleka shule.

Alitoa kauli hiyo Jijini Dodoma jana alipokutana na wafugaji kutoka wilaya saba za mkoa huo kwenye kikao cha kukaribishana na kufahamiana mkutano uliofanyika katika Ukumbi wa Jiji Dodoma.

Alisema mfugaji mwenye maendeleo ni yule aliyepeleka watoto shule kusoma na sivyo ilivyo sasa, mfugaji anaishi maisha ya kimaskini wakati anaposimama mfugaji ni tajiri mkubwa.

"Ni aibu kuona mfugaji ana ng'ombe zaidi ya 1,000, lakini maisha anayoishi ng'ombe ni sawa kabisa na maisha anayoishi mfugaji sasa hii ni aibu, nataka tutoke katika ufaugaji huu ili kila mfugaji maisha yake yabadilike.

"Itakuwa haina maana kuona mfugaji, anamsururu wa mifugo lakini bado ni maskini wa kutupwa, naomba mtambue kwamba mfugaji wa leo ni yule mwenye maendeleo, mwenye nyumba ya kisasa na watoto wake wote wenye umri wa kwenda shule wamekwenda shule," alisema Mtaka.

Pia aliwataka wafugaji hao, kuacha kufuga kizamani na badala yake kuanza kufuga kisasa ili waende sambamba na ujio wa makao makuu kwani mauzo yao hayatakuwa tena minadani.

Alisema baada ya kumalizika kwa Standaji Geji kutakuwa na viwanda vya kutosha hivyo wafugaji wataweza kuuza, maziwa, nyama na hata ngozi ndani ya Dodoma na nje ya Dodoma.

"Kumbukeni nyinyi ni wafugaji wa makao makuu ya nchi, nitashangaa sana endapo nitaona wafugaji kutoka mikoa mingine wanakuja kuchangamkia fursa ya soko katika Mkoa wetu wa Dodoma.

"Sasa niwaombe, tuachane na ufugaji wa kizamani, ufungaji wa kuwa na msururu wa n'gombe na ule wa kuhamahama hauna tija kwenu kwani hata mashamba yaliopo wazi, yatakwisha kwa sababu maeneo hayo mnayotegemea tunakwenda kuuza viwanja kwa wananchi wenye uhitaji wa maeneo," alisema.

ALiongeza kuwa; "Nitawakutanisha na wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo ili wawafundishe mbinu bora za ufugaji wa mifugo michache ila wenye faidi nyingi," alisema.

Awali wakitoa kero zao mbele ya Mkuu huyo wa Mkoa, wafugaji hao walisema changamoto yao kubwa wanayokabiliana nayo ni majosho na kutokuwepo kwa sehemu ya malisho ya mifugo yao.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji wenzake, Sadik Hassan kutoka Wilaya ya Kondoa, alisema kero yao kubwa ni sehemu ya malisho kwani karibu vijiji 18 wafugaji hawana sehemu ya kulishia mifugo yao hali inayosababisha migogoro ya ardhi kati yao na wakulima.

"Katika Wilaya yetu ya Kondoa, sisi wafugaji na wakulima tumeathiriwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kutokuwa na mawasiliono mazuri na viongozi wetu, kikubwa tunaomba maeneo ya malisho ya mifugo yetu," alisema.

Awali akisoma risala katika mkutano huo Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Dodoma, Reginaldo Lubeleje alimuomba Mkuu huyo wa Mkoa kuwatatulia migogoro iliyopo kati ya wahifadhi, wakulima na wafugaji hali iliyosababisha kukosa maeneo ya malisho.

Majira Uk.17, Tarehe 09/06/2021

Scanned with CamScanner

... Dar es Salaam, jana. (Picha na Jumanne Gude). ... maalumu ya uhandishi wa habari katika

# Wafugaji Moro walilia elimu matumizi sahihi ya viuatilifu

**NA WARIOBA IGOMBE,** *Morogoro*

KUKOSEKANA kwa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu katika mimea na wanyama, kumetajwa kuwa tatizo kubwa linalosababisha jamii ya wafugaji kula sumu bila kujua.

Hayo yalisemwa jana na wafugaji wakati wa jukwaa lililowakutanisha wafugaji, wakulima na viongozi wa serikali na kudai kuwa kitendo cha kutokuwa na elimu sahihi ya matumizi ya viuatilifu kutaleta athari kubwa nchini.

Adam Mwarabu ambaye ni miongoni mwa wafugaji hao, alisema baadhi ya wafugaji wamekuwa wakichoma mifugo yao sindano na ikitokea ng'ombe huyo anakufa humchinja na kula nyama yake bila kujali madhara ya dawa.

"Wengi hatuna uelewa wowote wa suala zima la matumizi ya viuatilifu vya mifugo, mimea na mazao jambo ambalo ni hatari kubwa kwa afya ya mlaji kwa ujumla hivyo tunaiomba serikali itusaidie ili tuepuka athari," alisema.

Alisema kitendo cha kula nyama ya ng'ombe aliyekufa huku akiwa anapatiwa matibabu ni sawa na kunywa sumu, jambo ambalo ni hatari kwa kuwa dawa hiyo kwa mwili wa binadamu ni sumu na madhara yake ni makubwa na kusababisha kifo.

Ole Mwarabu ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali linalowasaidia wafugaji na wakulima wadogo hapa nchini (PAICODEO) alisema kwa upande wa mazao wapo wakulima wanaonyunyizia dawa shambani bila kuwa na tahadhari.

"Utakuta mkulima ananyunyuzia viuatilifu vya kuzuia wadudu na magonjwa katika mimea shambani bila kuwa na vifaa maalumu mdomoni, puani na machoni kitendo hiki ni hatari kwani ile sumu humuathiri mkulima," alisema.

Mkulima wa kijiji cha Mvuha, Wilaya ya Morogoro, Ramadhani Mng'ongo, alikiri kutojua athari za matumizi ya viuatilifu shambani, hivyo aliiomba serikali na wadau wengine kwa ujumla kutoa ushirikiano ili wakulima wapate uelewa huo.

Alisema bila jitihada kufanyika watu wengi kuanzia mkulima hadi mlaji wanaweza kuwa hatarini kupata magonjwa yasiyoambukizwa kutokana na uelewa mdogo wa matumizi sahihi ya viuatilifu uliopo katika jamii.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, aliwaagiza maofika kilimo na mifugo kutoa elimu kwa wananchi ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima huku akiahidi kulifuatilia suala hilo kila wakati kwa kuwa ni la muhimu.

**Jitihada**

**ELIMU**

Elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu katika mimea na wanyama inapaswa kutolewa kwa jamii ya wafugaji kuepuka vifo

Uhuru Uk.18, Tarehe 09/06/2021

Scanned with CamScanner

# Ole Gabriel: Sasa tumeanza mwendo wa mashirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Sekta ya Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel amesema kwa sasa wameanza kwenda kwa mwendo wa mashirikiano baina ya Wizara ya Mifugo na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar katika kuhakikisha sekta hizo zinaendelea kupiga hatua kwenye kuhakikisha wafugaji wananufaika na mashirikiano waliojiwekea.

Pia amesema kupitia sekta hizo mbili kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar, wamekubaliana kuhakikisha wanaendeleza mashirikiano katika sekta hiyo kwa hali na mali, huku akihaidi kuwa hawatakuwa tayari kukwamisha mashirikiano hayo na watu waliopo katika sekta zao.

Ole Gabriel aliitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa maazimio ya kikao kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, ambapo alisema wamekubaliana kukutana kila robo ya mwaka katika kujadili mambo mbalimbali yanayoikabili sekta hiyo ya mifugo, huku wakitumia changamoto zitokanazo na sekta hiyo kuwa fursa.

Alisema kutokana na unyeti wa sekta hizo mbili ambazo ni moja ya sekta za uzalishaji na zinachangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi na kiwango cha chakula, hivyo wapo tayari kuhakikisha wanaimarisha mashirikiano hayo.

Katibu huyo alisema, wamekubaliana mambo mengine ikiwemo kuimarisha udhibiti wa uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, hususan nyama na maziwa ili kuimarisha sekta ya mifugo nchini.

"Tumekutana kwa lengo kubwa ambalo ni kuhakikisha tunatekeleza maelekezo ya Rais, Samia Suluhu Hassan ambaye ameelekeza kwamba hata kama sekta ikiwa si ya Muungano lakini inatumikia Jamuhuri ya Muungano, lazima iendeleze mashirikiano na hayo ndiyo tunatekeleza," alisema.

Alisema wamejadiliana kutatua changamoto za wafanyabiashara ikiwemo kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa vibali vya mazao ya mifugo, ambavyo vinatolewa Tanzania Bara vitakubalika Zanzibar huku vionavyotolewa Zanzibar vikubalike bara.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Maliasili Zanzbar, Maryam Juma Saadala alipongeza juhudi za serikali katika kukuza sekta ya mifugo nchini kwani sekta hiyo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi.

Maryam alisema maazimio hayo yafanyike kwa wakati kama walivyokubaliana na kukuza sekta hiyo kwa maendeleo ya nchi.

"Tutakuwa na mpango kazi wa pamoja katika kuimarisha ushirikiano na kutekeleza kwa vitendo," alisema.

Majira Uk. 16, Tarehe 09/06/2021

Scanned with CamScanner

# Jinsi ya kumlisha n'gombe anayekamuliwa ili kupata maziwa mengi

NA MWANDISHI WETU



WAFUGAJI walio wengi wanapenda kupata maziwa mengi, lakini hawazingatii kanuni na malisho kamili kwa ajili ya ng'ombe wao.

Ni muhimu kuzingatia kanuni. Ng'ombe wa maziwa wanahitaji virutubisho zaidi ili kuweza kuzalisha maziwa kwa wingi, hasa katika kipindi cha miezi 3-4 ya mwanzo baada ya kuzaa. Huu ni wakati ambao uzalishaji wa maziwa unakuwa juu.

Malisho ya ng'ombe wa maziwa ni lazima yawe na uwiano sahihi wa viungo. Mifugo inahitaji chakula kitakachowapa nguvu, protini, madini, na vitamin ili kujenga miili yao, kuzalisha maziwa, na kuzaliana. Kulisha ng'ombe wa maziwa kwa kutumia aina yoyote ya malisho haitoshi kukuhakikishia ng'ombe anakuwa na afya nzuri na kutoa maziwa ya kutosha.

Kama ilivyo kwa mifugo mingine kama kuku na hata binadamu, ng'ombe anahitaji mlo kamili. Vyakula vinavyohitajika kwa ng'ombe wa maziwa Malisho ya kijani Huu ni mlo mkuu kwa ng'ombe wa maziwa. Mlo huu ni muhimu na wenye virutubisho.

Malisho bora ya kijani ni yale yanayoweza kumpatia ng'ombe wa maziwa virutubisho muhimu vinavyohitajika. Malisho ya kijani yanatakiwa yawe ya kijani kibichi na machanga. Hii ina maana kuwa, majani ya malisho ni lazima yakatwe na kuhifadhiwa yakiwa bado machanga na kabla ya kuchanua. Hii ina maana kuwa mimea ambayo imepoteza rangi yake halisi ya kijani, inaweza tu kuwasaidia mifugo kuishi lakini haina virutubisho muhimu vya kuwapa mifugo nguvu, madini, protini na haiwezi kusaidia katika uzalishaji wa maziwa.

> **Malisho ya ng'ombe wa maziwa ni lazima yawe na uwiano sahihi wa viungo. Mifugo inahitaji chakula kitakachowapa nguvu, protini, madini, na vitamin ili kujenga miili yao, kuzalisha maziwa, na kuzaliana.**

Malisho yenye viwango vya chini vya virutubisho yanatakiwa yaongezewe kwa chakula cha ziada chenye kirutubisho vya kutosha kitakachoziba pengo la virutubisho vilivyokosekana. Vyakula vya kutia nguvu Kwa kawaida aina zote za majani ni chanzo kizuri cha vyakula vya kutia nguvu kwa mifugo, endapo yatalishwa yakiwa bado machanga. Mfano wa majani maarufu kwa malisho



ni matete, ukoka, majani ya tembo, seteria na guatemala.

Majani ya mahindi au mtama ni chakula kizuri sana kwa kuwapa nguvu mifugo. Vyakula vingine vinaweza kutokana na aina zote za nafaka, punje za ngano, au molasesi. Vyakula hivi vya kutia nguvu vinatakiwa vilishwe kwa kiasi kidogo.

Vyakula vya Protini Mimea michanga ina kiasi kikubwa cha protini kuliko mimea iliyokomaa. Mahindi machanga pamoja na majani ya viazi vitamu ni mahususi kwa protini. Mikunde ina protini nyingi zaidi kuliko nyasi. Mfano, mabaki ya majani ya maharagwe, njegere, desmodium na lusina. Majani yanayotokana na mimea kama lusina, calliandra au sesbania ina kiwango kikubwa cha protini pia. Aina nyingine ya vyakula vyenye protini ni mashudu ya pamba, mashudu ya alizeti na soya.

Tahadhari: Ng'ombe wa maziwa wasilishwe kwa kutumia aina zote za jamii ya mikunde kwa zaidi ya asilimia 30 ya uwiano wa mchanganyiko wa malisho ili kuepuka matatizo ya kiafya. Madini Ng'ombe wa maziwa wanahitaji madini ya ziada.

Madini ni lazima yapatikane muda wote, mfano kama jiwe la chumvi au chumvi ya unga ya kuweka kwenye (chakula) pumba. Wanyama wanaokuwa, wenye mimba, na ng'ombe anaenyonyesha wanahitaji kiasi kikubwa cha madini, mfano calcium na phosphorous kwa kuwa madini mengi yanatoka kwenye maziwa. Madini yanaweza kupatikana katika mimea ya jamii ya mikunde na mingineyo isipokuwa nyasi. Mimea hii inatoa kiasi kikubwa cha calcium na madini mengineyo.

